

**KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM
PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS – MIVUMONI
DAR ES SALAAM**

**MATANGAZO YA DOMINika YA KWANZA YA MAJILIO
MWAKA A TAREHE 26 NOVEMBA, 2022.**

Kristo...

MCHANGO WA PILI

Kwa ajili ya **UJENZI WA OFISI**. Jumuiya iandae vyombo, kwaya mtuongoze kwa wimbo.

NDOA

Bw. Erick Mpendaraha mtoto wa Melkior Gaspar na Epigenia Emili na Bi. Fides Pendo mtoto wa Camilius Ndewingia na Illuminata Sebastian.

Tangazo la kwanza.

Bw. Yuda Thadeus Lello mtoto wa Claudi John na Gratiana Peter na Bi. Liliana Mkabahati mtoto wa Silvani Gregory na Pudenciana Msuri.

Tangazo la Tatu na la mwisho.

Anayejua kizuizi cha Tangazo hili atoe taarifa ofisi ya mapadre.

TANGAZO KWA WASEMINARI WA ZAMANI

Mhashamu Jude Thaddaeus Ruwa'ichi anawaalika Waumini walei wote ambao walisoma na kupata malezi katika Seminary mbalimbali na wanaishi DSM kushiriki Misa maalumu ya kumshukuru Mungu kwa malezi ambayo waliyapata Seminarini. Baada ya Misa Askofu atapenda kuwa na mazungumzo na wote watakaoshiriki. Mahali na tarehe itakapofanyika Misa itatangazwa baada ya zoezi la kujianidikisha kukamilika. Washiriki ni wale tu ambao wamesoma au wamemaliza seminari ndogo kabla yam waka 2010 na ambao wamemaliza seminari kubwa kabla yam waka 2015.ili kujianidikisha fika ofisi ya H/ Walei Parokia.

MISA YA MAREHEMU WAZEE NA WASTAAFU

Kutakua na Misa Takatifu ya kuwaombea wazee na wastaafu marehemu wa Jimbo kuu la Dar es Salaam itakayoongozwa na Baba Mlezi wa Jimbo Fr. Benedict Shayo tarehe 30/11/2022 katika Parokia ya Manzese saa 11 jioni. Wahudhuriaji ni wazee na wastaafu wote wa Jimbo la Dar es Salaam. Viongozi wa wazee na wastaafu Parokia zote mnaombwa kuhamasisha wazee kuhudhuria Misa hiyo.

VIJANA

Kutakuwa na mazoezi ya igizo la Chrismass litakalofanyika kwa Masista De Paul, tunaomba vijana kushiriki kwa wingi na wazazi na walezi wanaombwa kuhamasisha.

CONSOLATA MISSION CENTRE-BUNJU

Wameandaa Semina ya siku tatu kwa vijana wadogo miaka 13-18 itakayofanyika Consolata Mission Centre Bunju kuanzia tarehe 8/12/2022 hadi tarehe 11/12/2022 kwa garama ya sh. 63,000 tu kwa kila kijana. Pia wameandaa Semina ya vijana wakubwa 18- 35 itayokuwa ya siku mbili kuanzia tarehe 9/12/2022 hadi 11/12/2022 itakayofanyika Consolata Mission Centre Bunju kwa gharama ya 33,000 kwa kila

kijana.Tunaomba kila Jumuiya ichangie vijana wadogo 2 na wakubwa 2. Kwa maelezo Zaidi wasiliana na viongozi wa vijana Parokia.

MAOMBI

Shirika la Tanzania Interfaith Partnership linawatangazia waumini wote kuwa kutakuwa na Tamasha la maombi kuombea Nchi kutohana na majanga mbalimbali ikiwemo ukame, ajali na magonjwa ya mlipuko.Kongamano hili litaongozwa na viongozi wa dini toka makanisa ya CCT, TEC, CCPTC na SDA.Mahali ni viwanja vya Mnazi mmoja siku ya tarehe 4 Disemba 2022 kuanzia saa 8:00 mchana wote mnakaribishwa kushiriki kongamano hilo.

HUDUMA YA MACHO

Upendo eye centre watakuwepo hapa Parokiani wakitoa huduma za macho Jumapili ya tarehe 4/12/2022 mara baada ya Misa.Watakuwa katika ukumbi wa Parokia wakitoa huduma za macho.Kwa wale wenye uhitaji mnaweza kuwaona hapo ukumbini kwa gharama nafuu.

UTOTO MTAKATIFU.

Uongozi wa Utoto Mtakatifu wanatoa shukrani zao za dhati kwa Baba Parooko, Kamati Tendaji, wazazi na waumini wote walioshiriki nao katika kuadhimisha miaka 25 ya Utoto Mtakatifu hapo jana hapa Parokiani.Mungu awabariki sana.

UJENZI WA OFISI

Plasta imemalizika, sasa kazi iko kwenye hatua ya kuweka floor.

HUDUMA KANISANI

Leo tunahudumiwa naJumuiya ya Mt. Marko Mwinjili Dominika ijayo tutahudumiwa na Jumuiya ya Yosefu Mfanyakazi Wakati huohuo Jumuiya ya Mt. Maria Goreti wajiandae.

MAUZO

Gazeti la Tumaini letu linapatikana kwenye duka la WAWATA kwa shilingi 1,000 tu.Jipatie nakala yako ilio sheheni habari kemkem

TUSIKILIZE SADAKA NA MATOLEO MENGINE DOMINIKA ILIYOPITA.

